

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA WAZIRI MKUU**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**WILAYA YA NYAMAGANA**

Anwani ya Simu:"ADMIN"

Simu:028-2501046

Unapojibu tafadhali taja:



06/03/2017

**TAARIFA KWA UMMA**

Ninatoa ufafanuzi kwa vyombo vya Habari ikiwemo Clouds FM ambao wamekuwa wakiuliza usahihi wa Taarifa iliyoandikwa na Gazeti moja lenye kichwa cha Habari DC AWASWEKA NDANI WATENDAJI KWA KUTOKUWA NA BARUA PEPE. Taarifa inadai kuwa Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana aliwasweka ndani kwa sababu ya kutokuwa na anuani ya Barua pepe. Mwandishi huyo pamoja na kumfafanulia suala hilo aliendelea na hitaji lake la kutoa taarifa isiyo sahihi. Hali ya matukio ikiwa kama ifuatavyo:

1. Tarehe 21/02/2017 Kaimu Mkuu wa Wilaya aliitisha kikao cha Wadau wa kupambana na Madawa ya kulevya wakiwemo waandishi wa Habari pamoja na StarTV na Watendaji hao wa Kata.. Kikao kilianza kwa sala kutoka kwa Kiongozi wa Dini ya Kiislamu na Kufungwa kwa sala na Kiongozi wa Dini ya Kikristo.
2. Katika Kikao hicho, tulianza kwa kusikiliza Hotuba iliyorekodiwa ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akifafanua vita dhidi ya Madawa ya kulevya,. Hotuba iliyorekodiwa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwa Vita dhidi ya madawa ya kulevya ijumuishe pia uuzaji wa pombe kali kwa kutumia viroba na Hatimaye Agizo la Mheshimiwa Makamu wa Rais kujumuisha vita hivyo sambamba na vita dhidi ya uvuvi Haramu.
3. Wawakilishi wa Chama cha Mapinduzi waliwasilisha Aya ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi inayohusu maelekezo kwa Serikali kuhusu mapambano dhidi ya Madawa ya kulevya.
4. Mwanasheria wa Jiji aliwasilisha mada ya sheria ya kudhibiti madawa ya kulevya ya Mwaka 2015.
5. Mganga Mkuu wa Jiji aliwasilisha Mada kuhusu madhara ya pombe kali kwenye mwili wa Binadamu

6. Afisa Uvuvi wa Jiji aliwasilisha mada kuhusu nyara haramu za uvuvi na uvuvi kwa kutumia sumu. Pia dalili za samaki aliyevuliwa kwa sumu na madhara yake kwa binadamu.
7. Baada ya mawasilisho hayo, kikao kilitoa maazimio mbalimbali baada ya kila makundi kuwasilisha namna ya kupambana na Madawa ya kulevya.
8. Kikundi cha Viongozi wa Dini kiliazimia kukutana tarehe 25/02/2017 kutoa tamko la kumuunga Mheshimiwa Rais katika Mapambano dhidi ya madawa ya kulevya na kualika wataalam kwenye makongamano ya Dini kuwasilisha mada hizo.
9. Vyombo vya habari vilitoa azimio la kuandaa makala ya kupambana na madawa wa kulevya na Radio IQRA iliamua kuanza mara moja kuanza mahojiano na Waliotoa mada kwenye kikao kuwafafanulia wananchi vita hiyo ya kupambana na Madawa ya Kulevya
10. Tarehe 23/02/2017 kaimu Mkuu wa Wilaya aliitisha kikao cha Kamati ya Usalama ya Wilaya na Kikosi kazi cha kila Kata cha Mapambano ya Madawa ya Kulevya ambavyo wenyeviti wake ni Watendaji wa Kata. Baada ya kupitia maelekezo ya Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa tulikubaliana Mpangokazi .

Tarehe 27/02/2017 ilipofika baadhi ya Watendaji wa Kata walikuwa hawajafungua Email address na Wala kuleta taarifa ya utekelezaji agizo la Mheshimiwa Rais la Kupambana na Madawa ya kulevya. Hivyo tuliitisha kikao cha dharura tarehe 28/02/2017 kuuliza kulikoni wamepuuza makubaliano ya kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais la wote kushiriki Mapambano dhidi ya Madawa ya Kulevya. Katika kikao ilionekana ni Watendaji 8 tu ndiyo waliotekeleza na 10 walikuwa wamekaidi.

Kwa kuwa Idara ya Polisi ina wataalam wa Teknolojia ya Mawasiliano tuliagiza wakatekeleze yafuatayo:

1. Watendaji kata wote 10 wakafungue Email addresses
2. Watendaji kata wote 10 wakaandae taarifa za Kata zao za Mapambano dhidi ya Madawa ya kulevya na Kumkabidhi Mkuu wa Polisi kabla ya saa 12.00 jioni kwani zilihitaajika na Kikosi kazi cha wilaya kwa ajili ya kufanya msako na kukamata watuhumiwa wa Madawa ya kulevya.

Hiyo ndiyo picha Halisi ya tukio hilo na kundi la Waandishi wa Habari lilikubaliana kurusha kwenye matangazo ya Mapambano dhidi ya Madawa ya kulevya kwa njia chanya.

Hivyo Mwandishi wa Habari hiyo hakulitendea haki kundi la Wanahabari waliokuwepo kwenye kikao chetu. Ninamshauri awasiliane na StarTv kupata Recorded Video ya Kikao hicho.

Tunaamini kwa sasa atakuwa pamoja na wengine katika kuandika taarifa chanya za Mapambano dhidi ya madawa ya kulevya.  
Ninaomba kuwasilisha

Dr Leonard Mosses Masale  
Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana